

Jina Dar Nam

102/2

KISWAHILI

Karatasi ya 2

LUGHA

Aprili 2013

Saa 2 ½

MTIHANI WA PAMOJA WA MOKASA

KISWAHILI

Karatasi ya 2

LUGHA

Saa 2 ½

Maagizo

Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.

Jibu maswali yote. Majibu yako yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	

Karatasi hii ina kurasa 10 zilizopigwa chapa.

Watahiniwa ni lazima wahakikishe kama kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

UFAHAMU (Alama 15)

Soma habari hii kisha jibu maswali yanayofuatia.

Uteuzi wa wagombea viti mbalimbali ulioisha juzi umefanyika katika hali ya kutatanisha kote nchini na kuacha wapiga kura tukijiuliza maswali mengi.

Uteuzi uliofikiriwa kuwa kazi rahisi kumbe sivyo. Matokeo yake ni kuwa mipango imefanywa na mambo mengi yametukia kuwa na dosari. Kwa mfano, nyaraka nyingi hazikuwa tayari kwa wakati wala hazikufikishwa katika vituo vya kura kwa wakati uliotakikana. Ndiyo maana zoezi ambalo lingefanyika kwa siku moja limechukua siku mbili na kujaa vurugu na mikanganyiko ambayo ingeepukwa. Sasa basi, ni jukumu la Tume ya Uchaguzi na Mipaka ya Maeneo Bunge (IEBC) kujiandaa vyema ili isije ikakumbwa na matatizo madogo kama hayo.

Milolongo mirefu ya wapiga kura inaweza pia kuepukwa kama idadi ya vyumba vya kupigia kura ingeongezwa. Ina maana pia kuwa rejesta ya wapiga kura ingetolewa nakala zaidi ili kuthibitisha kwa haraka na kuharakisha zoezi lenyewe.

Usalama katika vituo vya wapiga kura uimarishwe hasa sehemu ambazo kumekuwa na visa vya ajabu kwa mfano Malindi ambako kulizuka kituo bandia cha kupigia kura, Siaya ambako magari yalionekana yakisafirisha wahuni ambao wangetumika kuvuruga shughuli ya kupiga kura na kulifanyika vitendo vya kuwakosesha wananchi imani na mchujo wa viongozi.

Tumefurahi kuona polisi wakiwatia nguvuni mawakala wa wagombea viti waliokuwa wakigawa pesa kwa wapiga kura katika vituo mbalimbali. Hii ina maana wananchi wanahimizwa kufanya uchaguzi huru na wa haki. Hili ni muhimu kwa IEBC na wahakikishe kwamba wameliimarisha zaidi ifikapo Machi 4, mwaka huu tutakapokuwa na uchaguzi huru na wa haki.

Jambo jingine ambalo limejitokeza wazi ni kwamba wananchi wanahitaji sana elimu ya umma; wafundishwe kwa kina jinsi ya kupiga kura. Hili hasa linawahusu wale wasiojua kusoma na wasio na ufahamu mkubwa wa uchaguzi mkuu kulingana na katiba.

Wapiga kura wa aina hiyo huchukua muda mrefu katika kibanda cha kupiga kura na hatimaye wanaishia kutoka na kuwaendea watu wawasaidie. Huku ni kupoteza wakati na hupotoshwa kwa madai wanasaidiwa. Tunaomba sana vyombo vyote husika vitoe elimu ya kutosha mapema ili hali isije ikarudiwa katika uchaguzi mkuu unaonukia. Licha ya hayo, vifaa vyote muhimu viandaliwe mapema na kufikishwa kule vinakotakikana kuwa kwa wakati mwafaka ili kuepusha maajabu tuliyoshuhudia ya mambo kwenda upogo katika vituo vingi vya kupigia kura wakati wa uteuzi. Kadhalika, mawakala wa wawania viti katika ngazi mbalimbali wavalie mavazi rasmi ya vyama vyao ili kuepusha uwezekano wa kuwa na mawakala ghushi.

Maswali

a) Ipe habari hii kichwa mwafaka. (alama 1)

.....

b) Eleza ni dosari zipi zilizojitokeza wakati wa uchaguzi huu wa mchujo. (alama 4)

.....
.....
.....
.....
.....
.....

c) Mwandishi anatoa suluhisho gani kwa matatizo yaliyojitokeza katika zoezi hili la mchujo wa viongozi? (alama 4)

.....
.....
.....
.....

d) Fafanua juhudi ambazo zimefanywa na vyombo vya umma ili kutoa suluhu kwa mojawapo wa tatizo lililotajwa. (alama 1)

.....
.....

e) Mwandishi wa habari hii anaipa tume inayohusika na uchaguzi changamoto fulani ili kuufanikisha uchaguzi wa Machi 4. Zitaje. (alama 2)

.....
.....

f) Eleza maana ya maneno au ya vifungu vifuatavyo vya maneno: (alama 3)

i) Mawakala

.....

ii) Kwenda upogo

.....

iii) Ghushi

.....

UFUPISHO

(Alama 15)

Teknolojia mpya ni tawi la maarifa linalohusiana na Sayansi kwa upande mmoja na Uhandisi (Uinjini) kwa upande mwingine. Sayansi ni elimu inayotokana na uchunguzi na majaribio katika maabara. Nao uhandisi ni ujuzi wa kuunda mitambo. Maarifa ya sayansi yanapotumiwa kutengeneza vitu viwandani hali hii inakuwa teknolojia.

Zao mojawapo la teknolojia mpya ni simu tamba. Watu vijijini sasa wanawasiliana na jamaa zao walio mbali. Akina nyanya wanapopanda njugu, kupalilia migomba, kukama ngamia na kukuna nazi, wanaweza kuzungumza na wajukuu zao walio Uingereza, Uchina na kwingine kule. Hakuna mahali ambapo hapajafikiwa na teknolojia mpya. Tukitembelea baadhi ya nyumba tutaona vifaa kama vile tanuri la miale au mikrowevu ambalo linapika maharagwe yakaiva kwa dakika chache tu. Majokofu nayo yanawezesha kuhifadhi vyakula bila kuharibika. Hata maiti na mizoga inaweza kuhifadhiwa kwa miaka mingi kwa ajili ya utafiti bila kuoza katika ufuo wa mochari.

Kwa upande wa kilimo, teknolojia imefanya makubwa. La kustaajabisha ni mtu mmoja kulima eneo kubwa la shamba kwa trekta. Halafu akapanda kwa tandazi, akanyunyizia dawa kunyauha magugu, akavuna na kukoboa mahindi akiwa pekee yake. Siku hizi inawezekana kukuza mimea na kufuga wanyama wanaokomaa kwa muda mfupi na kutoa mazao maradufu kwa sababu ya teknolojia mpya. Teknolojia imewezesha watu kuvumbua aina nyingi za nishati. Badala ya kutegemea umeme unaotokana na maji tu, sasa watu wanatumia mvuke, nguvu za upepo na nishati ya jua kupata umeme. Kwa sababu hii hata mababu zetu vijijini wanatazama televisheni bila shida au wahka.

Kwa upande mwingine, teknolojia ina madhara yake. Kwa mfano, uundaji wa silaha kali unaendelea kuwaangamiza watu wengi. Mabomu ya kitoradi yaliyoangushwa Hiroshima na Nagasaki Japani mwaka wa 1945 ni zao la kisayansi. Haya yaliwaua watu wengi na madhara yake bado yanadhihirika hata leo katika maumbile ya watoto wanaozaliwa na upungufu. Tena magaidi na wahalifu wa kimataifa wanatumia teknolojia mpya kuimarisha mbinu zao za kutenda

maovu. Isitoshe, inawezekana kutumia teknolojia kuagiza benki kutuma pesa nje ya nchi bila mwenye hazina kujua.

Wahalifu wanaweza kusikiza mawasiliano ya watu kwa simu hata ikiwa ni baina ya polisi. Kisha matatizo mengi ya kiafya yasemekana yanatokana na vyakula vilivyokuzwa kwa kutumia teknolojia mpya. Katika usafiri, kuna gari moshi lenye kutumia stima badala ya makaa. Hili ni zao la teknolojia mpya vilevile. Ingawa mwendo wake ni wa kasi, kasi hiyo na stima huweza kusababisha ajali mbaya mno.

Maswali

(a) Fupisha aya ya pili na ya tatu. (maneno 70-80 alama 8)

Matayarisho

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Jibu

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

(b) Kwa kutumia maneno (55- 65) eleza mambo muhimu yanayoangaziwa kwenye aya ya 4 na 5. (Alama 7)

Matayarisho

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Jibu

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

For More Free KCSE Past Papers Visit www.freekcsepastpapers.com

MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)

a) Sauti /ny/ hutamkiwa wapi? (alama 1)

.....

b) Tunga sentensi moja ukitumia mofimu huru (alama 1)

.....

c) Tumia kihusishi cha wakati katika sentensi (alama 1)

.....

d) Ukizingatia kauli zilizo mabanoni, tunga sentensi ukitumia vienzi hivi (alama 2)

(i) Chomoa (kutenduka)

.....

(ii) Funga (tendama)

.....

e) Changanua sentensi hii kwa njia ya matawi. (alama 4)

Ambaye alifukuzwa jana asubuhi ni mtoto wa seremala

.....

.....

.....

.....

f) Onyesha matumizi mwafaka ya alama zifuatazo katika sentensi (alama 2)

(i) Mkwaju

.....

(ii) Mdokezo

.....

g) Geuza sentensi hii katika usemi halisi (alama 2)
Juma alimwamkua baba yake.

.....
.....

h) Bainisha shamirisho tofauti katika sentensi hii (alama 2)
Mchumba wake alipakuliwa chakula na Cheptoo.

.....
.....

i) Bainisha aina za vitenzi katika sentensi hizi (alama 2)
(i) Hao si watoto tena.

.....
.....

(ii) Anataka kuchora picha.

.....
.....

j) Tunga sentensi moja ili kuonyesha matumizi matatu tofauti ya kiambishi 'ki' (alama 3)

.....
.....
.....

k) Onyesha vishazi katika sentensi hii (alama 1)
Alipoenda nyumbani alimwona mtoto.

.....
.....

l) Tunga sentensi ukitumia kiwakilishi hiki (alama 1)
Gani

.....
.....

m) Kanusha sentensi hii kwa umoja. (alama 2)
Wanasiasa wanawachochea wachuuzi

.....

n) Tumia neno 'na' ili lilete dhana za vifupisho, wakati na umilikaji katika sentensi (alama 3)

.....

o) Tunga sentensi moja itakayoonyesha maana mbili tofauti za neno: Tema. (alama 2)

.....

p) Andika kinyume cha;
Wasichana hao wawili wamepatana. (alama 2)

.....

q) Kiambishi 'a' huonyesha kuwa nomino iliyotajwa ina mazoea ya kutenda kitendo. Eleza matumizi mengine kwa kutungia sentensi moja. (alama 2)

.....

.....

r) Tunga sentensi itakayodhihirisha matumizi ya kielezi cha idadi ya jumla. (alama 2)

.....

s) Andika ukubwa wa sentensi hii (alama 2)
Ngoma zikipigwa sana zitapasuka.

.....

t) Sahihisha sentensi hii (alama 1)
Angemripoti kwa mwalimu angalimjua mhalifu huyo.

.....

u) Nomino katika ngeli ya U-ZI zinaonyesha miundo kadhaa kama U – ny: Uzi – nyuzi.
Andika miundo mengine miwili na mifano mwafaka. (alama 2)

.....

.....

ISIMU JAMII (Alama 10)

Juma: Bwana Mwenyekiti naomba kuchangia kidogo. Ni muhimu kufahamu kuwa fonestemia ni kipengee katika sarufi ya nomino za lugha ya Kibantu Kiswahili kikiwamo. Kipengee hiki hakijafanyiwa utafiti

Amina: Asante sana Mwenyekiti, nakubaliana na Profesa Msanifu na utafiti wake. Hata hivyo, itakuwa pia muhimu kuelewa fika kuwa, katika muainisho wa kifonestemia ni baadhi tu ya silabi za neno hukaririwa...

Maswali

(a) Hii ni sajili ya aina gani. (alama 1)

.....

(b) Fafanua sifa za sajili uliyotaja hapo juu. (alama 4)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Pure: Dr Kilo, we have to meet our governor to discuss this matter.

Wimbi: You are right sir. I will arrange for the meeting. (*Anaingia mama mkongwe*)

Hujambo mama! Karibu katika zahanati yetu. Nikuhudumie vipi?

Mama: Sijambo mwanangu. Nahisi maumivu mengi kichwani tangu jana jioni.

(c) Huu ni mtindo gani wa lugha? (alama 1)

.....

(d) Eleza sababu za wazungumzaji kutumia mtindo huu wa lugha. (alama 4)

.....

.....

.....

.....

.....

.....